# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

**HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**

**MEI, 2026**

# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukwani,Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kutujaalia afya njema iliyotuwezesha leo hii kukutana katika kikao cha Kwanza cha Mkutano wa Tatu wa Baraza la Kumi na Moja kwa ajili ya kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara mbali mbali kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Kadhalika nakushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako madhubuti na busara unazoendelea kuzionesha katika kuendesha shughuli za Baraza hili Tukufu. Allah azidi kukupa nguvu wewe na wasaidizi wako muweze kuliendesha Baraza hili kwa uadilifu na umakini mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi, kwa kushinda kwa kishindo uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025 kwa asilimia 74.8, hii ni dhahiri wananchi wa Zanzibar wanaimani kubwa na uongozi wake thabiti, wenye maono na unaolenga kuimarisha utawala. Hali ambayo imeleta matumaini mapya kwa watumishi na wananchi kwa ujumla, aidha tunampongeza Mheshimiwa Rais kupitia uamuzi wake wa kuimarisha maslahi ya watumishi kwa kupandisha kima cha chini cha mshahara kutoka Shilingi Laki Tatu hadi kufikia Shilingi Laki Tano, hatua ambayo ni ya kihistoria na ya kujivunia kwa wafanyakazi wa Zanzibar.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee natoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais, ambaye ni kiongozi mkuu wa shughuli za Serikali katika Baraza la Wawakilishi, kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika kazi zake pamoja na uongozi wake mahiri na usimamizi wake wenye tija katika kuendesha shughuli za Baraza. Ameendelea kuonesha weledi na uwajibikaji katika kuratibu majukumu ya chombo hiki, jambo ambalo limechangia kwa kiasi kikubwa kuimarika kwa utekelezaji wa maamuzi ya Serikali. Kwa dhati kabisa, tunamuombea azidi kupata nguvu za kutekeleza majukumu yake kwa manufaa ya taifa letu.

**Mheshimiwa Spika,** kadhalika, tunatoa pongezi za dhati kwa Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratib na Baraza la Wawakilishi, Mheshimiwa Hamza Hassan Juma pamoja na watendaji wake wote kwa kujituma kwao na ushirikiano wanaoutoa katika kutekeleza majukumu yao ndani ya kamati yetu hasa katika kipindi hiki cha kuipitia bajeti hii, ameonesha ujasiri wa kazi jambo linalochangia kufanikisha malengo ya serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia, inatoa shukrani kwa watendaji wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao waliouonesha katika kazi yakupitia bajeti ndani ya Kamati hii. Ushiriki wao wa karibu, utayari wa kutoa ufafanuzi pamoja na mchango wao katika kujibu hoja mbalimbali zilizojitokeza, hususan zile zinazohusiana na mifumo ya fedha na bajeti ya serikali, umechangia kwa kiasi kikubwa kurahisisha kazi hii kuwa nyepesi kwa waheshimiwa wajumbe wa kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jukumu la msingi kwa mujibu wa Kanuni ya 101(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2024, Kamati ilikaa siku ya tarehe 21 Aprili 2026 kuchambua, kujadili na hatimaye kupitisha mapendekezo ya Serikali kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais – Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa mchakato huo, Waheshimiwa wajumbe walionesha umakini mkubwa kwa kuijadili bajeti hii na kuibua masuala muhimu ya msingi kwa dhamira ya kuhakikisha kuwa fedha zinazoidhinishwa na Kamati zinatumika kama ilivyokusudiwa. Aidha, juhudi hizo zililenga kuimarisha misingi ya uwajibikaji na nidhamu katika matumizi ya fedha za umma kwa maslahi ya taifa.

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuendelea na hotuba hii, kwa ruhusa yako na kwa heshima ya kipekee, naomba nichukue fursa hii kuwatambua Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kama ifuatavyo:

1. Mhe: Machano Othman Said - Mwenyekiti
2. Mhe: Aza Januar Joseph - M/Mwenyekiti
3. Mhe: Zaina Abdulla Salum - Mjumbe
4. Mhe: Mmanga Mohammed Hamed - Mjumbe
5. Mhe: Masoud Amour Masoud - Mjumbe
6. Mhe: Mahmoud Shineni Ali - Mjumbe
7. Mhe: Mahfoudh Abdalla Mohammed - Mjumbe
8. Ndg: Ali Alawy Ali - Katibu
9. Ndg: Mwanaisha Mohammed Kheir - Katibu
10. Ndg. Shawana Mohammed Haji - Katibu
11. Ndg. Amina Abeid Hemed - Mkalimani
12. Ndg. Hassan Lila Mrisho - Afisa Bajet

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 103 (6) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2024, naomba kuwasilisha Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Maoni ya Kamati ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kama ifuatavyo.

**Mheshimiwa Spika, k**wa kuwa Ofisi ya makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi imeundwa na baadhi ya Taasisi zinazojitegemea kimafungu. Hivyo, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 wizara hii itatekeleza kazi zake kupitia mafungu makuu matatu (3) ya kibajeti, ambayo ni Fungu 003 – Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Fungu 020 Afisi ya Baraza la Wawakilishi na Fungu 031 Tume ya Uchaguzi ambayo kwa mwaka 2026/2027 itaendelea kutekeleza na kusimamia Programu Kuu 7 na Programu Ndogo 14 zitakazojumuisha shuhuli zote zilizopangwa kufanywa ndani ya mwaka huu wa fedha kama inavyoonekana katika kitabu kikuu cha Bajeti.

**PROGRAMU KUU YA URATIBU WA SHUGHULI ZA SERIKALI**

**Mheshimiwa Spika,** kupitia programu ndogo ya kukabiliana na maafa kwa lengo la kujenga uhimili wa jamii katika kukabiliana na maafa na athari zake kwa ujumla, na kwakua maafa ni tukio la hatari linaloweza kusababisha uharibifu au madhara makubwa kwa watu, mali na mazingira. Hivyo, kunahitajika msaada wa ziada ili kukabiliana nayo. Katika kutekeleza majukumu yake, kupitia **Programu Ndogo hii ya S0030201 ya Kukabiliana na Maafa,** Kamati inaipongeza Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar kwa juhudi inazoendelea kuzichukua, ikiwemo kufanikisha kufanyika kwa vikao vya kukabiliana na maafa pamoja na vikao vya Kamati ya Kitaalam ya Kitaifa ya Kukabiliana na Maafa. Hatua hii inaonesha dhamira ya kuimarisha uratibu na utayari wa kujikinga na kukabiliana na majanga katika ngazi mbalimbali za kiutawala nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi hizo, Kamati inaitaka Kamisheni kuhakikisha kuwa inafanya juhudi za makusudi kwa kuwashirikisha waheshimiwa wawakilishi katika vikao vya kamati za maafa, kwa kuwa wao ni wadau muhimu na waangalizi wakubwa wa majimbo yao, hivyo ushiriki wao utachangia kupanga na kutekeleza mikakati ya kukabiliana na majanga mbali mbali kwa urahisi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine, Kamati imeona kuna umuhimu mkubwa wa kupata taarifa za kina kuhusu maendeleo ya Mfuko wa Maafa, ikiwa ni pamoja na hatua iliyofikiwa ya kuanzishwa au kuimarishwa kwake, ili kuhakikisha uwepo wa rasilimali za uhakika kwa ajili ya kukabiliana na majanga mbali mbali katika jamii. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha uwezo wa Kamisheni, ili iweze kukabiliana na changamoto zinazotokana na majanga ya asili na yale yanayosababishwa na binadamu katika nyakati tofauti.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wa Ofisi ya sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa katika kuwaenzi viongozi wa taifa letu kwa juhudi kubwa wanazochukua katika utoaji wa huduma bora na zenye ufanisi na kwa kuzingatia malengo ya maendeleo ya Zanzibar. Kamati inapenda kuipongeza ofisi hii kwa juhudi zake katika kuratibu shughuli mbalimbali za sherehe za kitaifa. Kupitia **Programu Ndogo ya S0030202** inayohusu Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa**,** Kamati imeridhika na Idara hii kwa kazi nzuri ya kuratibu wiki ya kuwaenzi viongozi wa kitaifa, ambayo ina mchango mkubwa katika kuenzi historia na tunu za taifa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi hizo, Kamati inasikitishwa na hali ya miundombinu ya barabara zinazoelekea katika makaburi ya kuwaenzi viongozi hao. Kwani kumekuwepo na changamoto ya kukosekana au ubovu wa baadhi ya barabara hizo, zinazosababisha usumbufu mkubwa hasa wakati wa kipindi cha mvua ambacho huambatana na maadhimisho ya wiki ya kuwaenzi viongozi hao. Kutokana na hali hiyo. Kwa mara nyengine tena, Kamati inaiomba Serikali kuchukua hatua za makusudi kulipatia ufumbuzi suala hili ambalo limekuwa likijirudia kwa muda mrefu, ili kuwezesha wananchi na viongozi kufika katika maeneo hayo kwa urahisi na kwa hadhi inayostahili.

**Mheshimiwa Spika,** katika **Programu Ndogo ya S0030203** inayohusu Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kamati imeridhishwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) kutokana na ufanisi wake mkubwa

uliopatikana katika awamu iliyopita chini ya uongozi wa Mkurugenzi Mtendaji, Ndugu Shadrack Mzirai, kwa juhudi anazoendelea kuzichukua katika kuimarisha ustawi wa jamii na kuwawezesha wananchi kiuchumi, hususan kaya zenye hali ngumu ya kiuchumi. Hatua hii inaonesha mwendelezo thabiti wa dhamira ya Serikali katika kupunguza umasikini kwa kuongeza nguvu katika maisha ya wananchi.

**Mheshimiwa Spika;** sambamba na mafanikio hayo, Kamati inashauri katika awamu yake ya Tatu (TASAF III), kuimarishwa zaidi kwa mifumo ya usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu hii, ili kuhakikisha malengo yaliyokusudiwa yanawafikia walengwa kwa wakati na kwa kiwango kinachotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Idara ya Uhamiaji Zanzibar, Kamati inaipongeza kwa jitihada zake za kuimarisha utoaji wa huduma kwa wageni na wananchi wa Zanzibar pamoja na utekelezaji wa miradi yake muhimu ya maendeleo. Pamoja na hayo, Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kukamilisha kwa wakati ujenzi wa Ofisi ya Uhamiaji ya Wilaya ya Mjini Magharibi, kwani ucheleweshaji wa mradi huu unaathiri utoaji wa huduma kwa wananchi na wageni pamoja na kupungua kwa ufanisi wa kiutendaji wa Idara hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inathamini juhudi za kazi wanazifanya Ofisi ya Uratibu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) iliyopo Dodoma kwa juhudi zake za kuendelea kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha uwakilishi wa Zanzibar katika ngazi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hata hivyo, Kamati inaona umuhimu wa kuongezwa kwa rasilimali fedha na vifaa ili kuiwezesha Ofisi hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi, hususan katika kulinda na kusimamia maslahi ya Zanzibar kwenye masuala ya Muungano ambayo yanahitaji ufuatiliaji wa karibu na wa mara kwa mara.

**PROGRAMU KUU YA KUTUNGA SHERIA, KUPITISHA BAJETI NA KUSIMAMIA TAASISI ZA SERIKALI NA PROGRAMU KUU YA UONGOZI NA UTAWALA WA BARAZA LA WAWAKILISHI**

**Mheshimiwa Spika,** kwenye Fungu la 020, Baraza la Wawakilishi linaendelea kutekeleza wajibu wake wa msingi wa kutunga sheria, kusimamia Serikali na kuwakilisha wananchi. Kamati inatambua umuhimu wa kuimarisha taasisi hii ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa wepesi zaidi, hususan uimarishaji wa demokrasia na utawala bora.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inalipongeza Baraza la Wawakilishi kupitia **Programu Kuu ya Uongozi na Utawala wa Baraza la Wawakilishi (O2002)** kwa juhudi zake za kutoa mafunzo kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi la Kumi na Moja pamoja na wafanyakazi wa Afisi ya Baraza, hatua inayochangia kuimarisha utekelezaji wa majukumu yao. Licha ya hayo, Kamati inaitaka Afisi ya Baraza kuendeleza utaratibu wa kuwapatia mafunzo wajumbe na watendaji wake kadri hali itakavyoruhusu, ili kuendelea kuwajengea uwezo katika kushughulikia majukumu yanayowakabili.

**Mheshimiwa Spika,** mbali na hayo, Kamati imefurahishwa na uamuzi wa Serikali kuanza utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa majengo mapya ya Baraza la Wawakilishi katika eneo la Kisakasaka – Unguja. Hii ni hatua muhimu katika kuboresha mazingira ya kazi ya taasisi hii muhimu. Pamoja na juhudi hizo, Kamati inaiomba Serikali kuharakisha mchakato wa ulipaji fidia kwa wananchi wa maeneo husika ili kupisha ujenzi huo kuanza kwa wakati, jambo litakalosaidia kupunguza changamoto ya uhaba wa kumbi za mikutano pamoja na ofisi kwa wafanyakazi wa Afisi ya Baraza.

**PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI WA SHUGHULI ZA UCHAGUZI**

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Uchaguzi yenye Fungu **021** ina jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli zote za uchaguzi kwa mujibu wa sheria. Kamati inaona umuhimu wa kuendelea kuimarisha uwezo wa Tume hii ili

kuhakikisha kuwa uchaguzi unakuwa huru, wa haki na wenye kuaminika, unaozingatia kikamilifu misingi ya kidemokrasia.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhishwa na jitihada za Serikali katika kuimarisha miundombinu ya majengo ya Afisi za Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar. Katika kuendeleza juhudi hizo, Kamati inaiomba Serikali kuidhinisha jumla ya Shilingi Bilioni Sita, Milioni Mia Tano na Kumi na Moja na Laki Mbili (6,511,200,000) ili kuwezesha kuendelea kwa shughuli za uratibu na usimamizi wa mradi wa ujenzi wa Afisi za Tume katika ngazi ya wilaya.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hilo, Kamati inaitaka Tume kuendeleza utoaji wa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uchaguzi katika vipindi vyote, badala ya kusubiri hadi wakati wa kampeni, ili kuongeza uelewa na ushiriki wa wananchi katika mchakato mzima wa kidemokrasia.

**Hitimisho**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na juhudi zinazofanywa na taasisi hizi, Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa, zikiwemo upungufu wa rasilimali fedha, ucheleweshaji wa utoaji wa fedha, uhaba wa watumishi wenye ujuzi maalum, pamoja na changamoto za uratibu kati ya taasisi mbalimbali. Kutokana na hali hiyo, Kamati inapendekeza Serikali kuhakikisha upatikanaji wa bajeti ya Ofisi hii na taasisi zake ya Shilingi Bilioni Mia Moja na Thelathini na Tano, Milioni Mia Sita na Sabiini na Sita, Laki Nne na Thamanini na Nane, Mia Moja na Thamanini na Sita (135,676,488,186) kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inapatikana kwa ukamilifu na utoaji wa fedha kwa wakati, ili kuwezesha kuimarishwa kwa rasilimali watu kupitia ajira na mafunzo, sambamba na kuboresha mifumo ya uratibu wa taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maoni na mapendekezo yaliyotolewa, Kamati inaunga mkono Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa

mwaka wa fedha 2026/2027, huku ikisisitiza umuhimu wa kuyatekeleza kikamilifu mapendekezo hayo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Baraza la Wawakilishi, Ndg. Raya Issa Mselem kwa kuwangoza vyema watumishi wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Baraza hili ikiwemo vikao vya kamati pamoja na maandalizi mazuri ya kikao hiki cha bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Baraza lako Tukufu liunge mkono hoja kwa kuichangia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha.

…………………………………

(Mhe. Aza Januar Joseph)

M/Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR